## SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO NA MIFUGO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

### MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**KUANZISHWA KWA TAASISI YA UTAFITI**

3. Kuanzishwa kwa Taasisi.
4. Nembo na muhuri wa Taasisi.
5. Kazi za Taasisi.

**SEHEMU YA TATU**
**USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA TAASISI**

6. Kuanzishwa na muundo wa Bodi.
7. Sifa za Mwenyekiti wa Bodi.
8. Kazi za Bodi.
9. Uwezo wa Bodi.
10. Katibu wa Bodi.
11. Mwenendo wa Bodi.
12. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.
13. Uteuzi wa Naibu Mkurugenzi Mkuu.
14. Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

15. Idara, vitengo na divisheni.

16. Wafanyakazi wa Taasisi.

## SEHEMU YA NNE
## UENDESHAJI WA UTAFITI

17. Kuidhinisha utafiti.

18. Utafiti unaofanywa na mtafiti binafsi.

19. Usajili wa mtafiti.

20. Usajili wa utafiti au miradi ya utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu.

21. Mali Bunifu.

22. Taarifa.

23. Uchapishaji wa matokeo ya utafiti.

24. Matumizi ya wanyama katika majaribio.

25. Uhamishaji wa sampuli.

## SEHEMU YA TANO
## KUANZISHWA KWA KAMATI YA MAADILI YA UTAFITI

26. Kuanzisha na muundo wa Kamati ya Maadili ya Utafiti.

27. Kazi za Kamati ya Maadili ya Utafiti.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA FEDHA

28. Fedha na Rasilimali za Taasisi.

29. Bajeti ya Taasisi.

30. Hesabu na Ukaguzi.

31. Uwezo wa kuwekeza.

32. Ripoti ya mwaka ya Taasisi.

33. Ufunguaji wa hesabu za benki.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

34. Makosa na adhabu.

35. Adhabu ya ziada.

36. Kumaliza kosa.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

37. Rufaa.

38. Uwezo wa kurekebisha Jadweli.

39. Kanuni.

40. Kufuta na kubakiza.

## JADWELI

**SHERIA NAM. 6 YA 2024**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

......06 | 10 |......, **2024**

# SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO NA MIFUGO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar, 2024 na itaanza kutumika baada ya kuwekwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"aina" maana yake ni kundi la mimea lenye sifa za aina moja katika daraja la chini ambalo linaweza:

(a) kuchukuliwa kama aina kuhusiana na kufaa kwake kwa kupandikizwa bila ya kubadilika;

(b) inafahamika kwa kuonesha sifa zitokanazo na matokeo ya kinasaba au mchanganyiko wa vinasaba; au

(c) kutofautishwa kutokana na sehemu ya mmea kwa kuonesha angalau moja ya sifa zilizotajwa.

"baioteknolojia" maana yake ni matumizi ya mifumo ya kibaiolojia ya uzalishaji au usarifu wa bidhaa au huduma;

"benki ya viinitete" maana yake ni hazina halisi katika eneo moja au zaidi ambapo sampuli za vinasaba vya wanyama au mimea vinahifadhiwa au kuwekwa na inajumuisha wanyama hai, mimea, viinitete, mayai ya vimelea, mbegu za mazao, mbegu za kiume, mbegu za kike na sehemu nyengine za mnyama au mmea zenye vinasaba;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6(1) cha Sheria hii;

"kabila" maana yake ni kundi miongoni mwa aina ya wanyama ambao wana alama na muonekano maalumu, na waliozalishwa mahsusi kwa matumizi maalumu;

"Kamati ya Maadili ya Utafiti" maana yake ni Kamati ya Maadili ya Utafiti ya Taasisi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 26(1) cha Sheria hii;

"kilimo" maana yake ni sayansi, taaluma au kazi za kilimo na uoteshaji wa mazao ikijumuisha mazao ya misitu katika viwango tofauti vya uandaaji na uuzaji wa bidhaa zinazooteshwa;

"maabara" maana yake ni jengo la maabara ya utafiti lenye vifaa na wataalamu wenye uweledi;

"maradhi" maana yake ni mabadiliko yoyote kutoka hali ya kawaida ya mwili wa mnyama au mmea na inajumuisha dalili na muonekano wa maradhi;

"mfugaji" maana yake ni mtu anayemiliki au anayesimamia mifugo na kutumia teknolojia za uzalishaji mifugo;

"mifugo" maana yake ni wanyama wa nchi kavu wanaofugwa ili kutoa aina mbalimbali za bidhaa na huduma kama vile nguvukazi, nyama, maziwa, mayai, ngozi, nyuzi na manyoya;

"mnyama" maana yake ni kiumbe yoyote wa nchi kavu mwenye uti wa mgongo au asiyekuwa na uti wa mgongo asiyekuwa binadamu;

"mkulima" maana yake ni mtu anayemiliki, anayesimamia au anayelima shamba kwa kutumia teknolojia za kilimo;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 12(1) cha Sheria hii;

"mradi wa utafiti" maana yake ni shughuli za utafiti ambazo zinajumuisha utafiti zaidi ya mmoja;

"mtafiti" maana yake ni mtu anayefanya utafiti wa kitaaluma au kisayansi kuhusiana na kilimo, mifugo au rasilimali za misitu;

"Naibu Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 13(1) cha Sheria hii;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"rasilimali za misitu" inajumuisha miti, wanyamapori, mimea, mjumuiko wa baioanuwai, ufugaji nyuki na bidhaa zake na rasilimali nyengine zenye uhai na zisizo na uhai ambazo hutoa hifadhi, makaazi au chakula ambazo zinahusiana na mfumo wa ikolojia ya misitu;

"sampuli" maana yake ni kifaa ambacho kinakusanywa kwa madhumuni ya utafiti;

"Taasisi" maana yake ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3(1) cha Sheria hii;

"utafiti" maana yake ni utaratibu wa uchunguzi wa kimfumo unaojumuisha ukusanyaji wa taarifa, uwekaji wa kumbukumbu wa taarifa muhimu, uchambuzi na tafsiri ya taarifa hizo kwa mujibu wa mbinu zinazofaa zilizowekwa kwa fani za kilimo, mifugo au msitu na nyanja za kitaaluma ili kuendeleza, kuhakiki na kusambaza teknolojia;

"wadudu" maana yake ni jamii yoyote ya viumbe, kinasaba au aina ya kibaiolojia ya mmea na mnyama au kiumbe kinachodhuru mimea, wanyama au mazao ya mmea na mnyama;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya kilimo na mifugo;

"zao" maana yake ni mbegu iliyopandwa au iliyojiotea wenyewe au zao la kilimo au zao lililosarifiwa.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA TAASISI YA UTAFITI

Kuanzishwa kwa Taasisi.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Taasisi itakayojulikana kama Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar na ufupisho wake utakuwa "ZALIRI".

(2) Taasisi itakuwa ni chombo kinachojitegemea chenye kurithiwa na itakuwa na muhuri wake, na kwa mujibu wa sheria zinazotumika, kwa jina lake, itakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua na kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba, makubaliano au muamala wowote;

(d) kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka katika taasisi yoyote ya fedha; na

(e) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo lolote ambalo Taasisi kwa asili yake inaweza kutekeleza kwa mujibu wa sheria.

Nembo na muhuri wa Taasisi.

**4.**-(1) Kutakuwa na nembo na muhuri wa Taasisi katika umbo na namna itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya nembo na muhuri wa Taasisi katika waraka wowote yataidhinishwa na saini ya Mkurugenzi Mkuu au Afisa mwengine yeyote wa Taasisi aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Muhuri wa Taasisi utakuwa chini ya uangalizi wa Mkurugenzi Mkuu au mtu mwengine kama Mkurugenzi Mkuu atakavyoelekeza.

(4) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Taasisi utawekwa muhuri wa Taasisi na utathibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Taasisi.

**5.**-(1) Taasisi itaendesha, itasimamia, itafuatilia na itaratibu utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu ndani ya Zanzibar.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya ujumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Taasisi:

(a) itaendesha utafiti wa mazao, misitu, mifugo, vinasaba asili, baioteknolojia na bidhaa zake kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii;

(b) itapanga, itaendesha, itakuza, itaratibu utafiti na kuzifanya kuwa za kibiashara na kusambaza matokeo ya utafiti;

(c) itafanya kazi kwa kushirikiana na taasisi za umma, asasi za kiraia, sekta binafsi, jumuiya za wakulima na wafugaji zinazohusiana na ubunifu wa utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu;

(d) itaweka miongozo ya utoaji huduma za utafiti zikiwemo viwango vya utafiti, kanuni za maadili, mwenendo na vitendo;

(e) itatoa, itaendesha na itakuza huduma za ushauri katika maeneo ya utafiti, mafunzo na usambazaji wa taarifa za uzalishaji kwenye kilimo, mifugo na rasilimali za misitu, afya na sayansi zinazowiana;

(f) itatunza na kuhifadhi taarifa zinazohusiana na utafiti wa kilimo, mifugo au rasilimali za misitu kutoka kwa watafiti, taasisi na wadau wengine;

(g) itachapisha matokeo ya utafiti katika majarida, miongozo, makala, taarifa na maandiko mengine yanayofaa;

(h) itasajili watafiti muhimu wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu katika sekta za umma na binafsi, na kulitunza daftari la kumbukumbu la utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu;

(i) itaweka na kuhifadhi benki ya viinitete kwa lengo la kuainisha, kutathmini, kuhifadhi na kuendeleza mimea, wanyama na rasilimali za vinasaba vya malisho;

(j) itapendekeza kuhusiana na matumizi ya baioteknolojia kwa maendeleo ya kilimo, mifugo au rasilimali za misitu;

(k) itashirikiana na taasisi za ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa katika kufanya utafiti wa mazao, misitu, mifugo, vinasaba asili, baioteknolojia na bidhaa zake;

(l) itaharakisha upatikanaji wa taarifa za utafiti, rasilimali na teknolojia kwa kukuza matumizi ya matokeo ya utafiti na teknolojia katika fani za kilimo, mifugo na rasilimali za misitu;

(m) itaishauri Serikali katika masuala yote yanayohusiana na utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu;

(n) itasaidia, itahamasisha na kuendesha shughuli za kujenga uwezo kuhusiana na utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu; na

(o) itafanya kazi nyengine yoyote kwa lengo la utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA TAASISI

Kuanzishwa na muundo wa Bodi.

**6.**-(1) Kunaanzishwa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Mkurugenzi anayehusika na utafiti katika Wizara inayohusika na kilimo na mifugo;

(d) mwakilishi mmoja kutoka taasisi ya elimu ya juu inayohusika na kilimo, mifugo au maliasili; na

(e) wajumbe watatu kutoka jumuiya zilizosajiliwa zinazohusiana na kilimo, ufugaji na usimamizi wa misitu.

(2) Wajumbe chini ya kifungu kidogo cha (1)(d) na (e) cha kifungu hiki watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia sifa zifuatazo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya kilimo, rasilimali za misitu, utibabu wa wanyama au sayansi ya wanyama; na

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika fani hiyo.

Sifa za Mwenyekiti wa Bodi.

7. Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya pili katika fani ya kilimo, rasilimali za misitu, utibabu wa wanyama au sayansi ya wanyama kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika sekta ya umma au sekta binafsi; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Bodi.

**8.** Kazi za Bodi zitakuwa ni:

(a) kusimamia kazi zote za Taasisi;

(b) kuhakikisha kuwa kazi za Taasisi zinaendana na sera, malengo na vipaumbele vya Ajenda ya Utafiti ya Zanzibar;

(c) kuidhinisha na kutathmini katika muendelezo wa programu zinazotekelezwa na Taasisi;

(d) kutoa maelekezo kama inavyohitajika katika masuala yote yaliyomo ndani ya mamlaka ya Taasisi; na

(e) kuhakikisha kuwa fedha na rasilimali za kutosha zinapatikana kwa Taasisi ili kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Uwezo wa Bodi.

**9.** Bodi itakuwa na uwezo wa:

(a) kuidhinisha bajeti ya mwaka ya Taasisi;

(b) kupendekeza muundo wa Taasisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(c) kuajiri, kupandisha daraja au kuteua wafanyakazi wa Taasisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(d) kupitia na kuidhinisha sera, mikakati, mipango kazi, miongozo, ripoti, taratibu za uendeshaji, ada na tozo za Taasisi; na

(e) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mfanyakazi yeyote kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 au Kanuni zake.

Katibu wa Bodi.

**10.**-(1) Bodi itateua mfanyakazi wa Taasisi kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria au ana sifa ya kuwa katibu wa shirika kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali; na

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano katika utumishi wa umma.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na:

(a) ataanda ajenda za vikao vya Bodi kwa kushauriana na Mwenyekiti;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza kumbukumbu sahihi na zenye kujitosheleza za vikao za Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi na kwa wakati za vikao vya Bodi kwa wajumbe; na

(e) atatekeleza kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Mwenendo wa Bodi.

**11**. Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yatakuwa kama yalivyoelezwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

**12**.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya pili katika fani ya sanyansi ya kilimo, rasilimali za misitu, utibabu wa wanyama au sayansi ya wanyama kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba ndani ya sekta ya umma au binafsi katika mambo yanayohusiana na utafiti wa kilimo, mifugo au rasilimali za misitu;

(c) amechapisha machapisho ya utafiti yanayokubalika yasiyopungua manne ya kilimo, mifugo au rasilimali za misitu katika majarida yanayopitiwa; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

Uteuzi wa Naibu Mkurugenzi Mkuu.

**13**.-(1) Kunaweza kuwa na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu ikiwa ana sifa na uweledi sawa wakuteuliwa kama Mkurugenzi Mkuu.

(3) Naibu Mkurugenzi Mkuu atakuwa Msaidizi Mkuu wa Mkurugenzi Mkuu.

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

**14**.-(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi na atawajibika na kazi za kila siku za Taasisi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu:

(a) ataiongoza Taasisi katika kupanga na kutekeleza utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu kwa maendeleo;

(b) ataendesha, atadhibiti na kusimamia mali za Taasisi;

(c) atawezesha utekelezaji wa programu za utafiti na tathmini zake;

(d) ataanzisha na kutunza daftari la kumbukumbu la watafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu kutoka katika sekta ya umma au binafsi na miradi yao ya utafiti;

(e) atasajili watafiti wa umma na binafsi na tafiti zao; na

(f) atafanya kazi nyengine yoyote kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii.

Idara, vitengo na divisheni.

**15.**-(1) Taasisi, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa kazi zake chini ya Sheria hii, itaanzisha idara, vitengo na divisheni kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Wakuu wa idara na vitengo watateuliwa na Bodi kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(3) Wakuu wa divisheni watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Wakuu wa idara, vitengo na divisheni watawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu.

Wafanyakazi wa Taasisi.

**16.** Kutakuwa na wafanyakazi wa Taasisi watakaoajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

## SEHEMU YA NNE
## UENDESHAJI WA UTAFITI

Kuidhinisha utafiti.

**17.**-(1) Endapo utafiti utafanywa na:

(a) Taasisi, utaidhinishwa na Bodi; na

(b) mtafiti binafsi, utaidhinishwa na Kamati ya Maadili ya Utafiti.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "mtafiti binafsi" inajumuisha mtu binafsi, taasisi au shirika.

Utafiti unaofanywa na mtafiti binafsi.

**18**.-(1) Mtu anayetaka kufanya utafiti juu ya suala lolote linalohusiana na kilimo, mifugo au rasilimali za misitu ataomba idhini ya maadili kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu.

(2) Namna ya maombi na uidhinishaji kwa watoaji huduma za utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu na mambo mengine yoyote yanayohusiana na hayo yataainishwa katika kanuni.

(3) Mtafiti ambaye pendekezo lake limeidhinishwa chini ya Sheria hii atalazimika kuipatia Taasisi ripoti ya maendeleo ya utafiti katika vipindi kama ambavyo Taasisi inaweza kuamua.

(4) Mtu ambaye atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

Usajili wa mtafiti.

**19**.-(1) Mtu hatatoa huduma ya utafiti au kufanya utafiti chini ya Sheria hii isipokuwa mtu huyo awe amesajiliwa na Mkurugenzi Mkuu.

(2) Mtu ambaye atatoa huduma ya utafiti au kufanya utafiti bila kusajiliwa kwa mujibu wa kifungu hiki, ametenda kosa.

Usajili wa utafiti au miradi ya utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu.

**20**.-(1) Mtu hatatekeleza utafiti au mradi wa utafiti wa kilimo, mifugo au rasilimali za misitu isipokuwa utafiti au mradi huo umesajiliwa na Mkurugenzi Mkuu.

(2) Mtu anayekusudia kusajili utafiti au mradi wa utafiti wa kilimo, mifugo au rasilimali za misitu atawasilisha maombi kwa Mkurugenzi Mkuu kwa namna kama ilivyoelezewa katika kanuni.

(3) Mkurugenzi Mkuu anaweza kusajili utafiti au mradi wa utafiti wa kilimo, mifugo au rasilimali za misitu kwa namna na kwa kuzingatia masharti kama yalivyoelezwa katika kanuni.

(4) Mtu anayefanya utafiti au mradi wa utafiti wa kilimo, mifugo au rasilimali za misitu ambao haujasajiliwa kwa mujibu wa kifungu hiki, ametenda kosa.

Mali Bunifu.

**21**.-(1) Endapo utafiti wowote unatumia fedha za umma au kwa niaba ya Taasisi, kitu chochote kitakachogundulika au kubuniwa kitakuwa ni mali ya Taasisi.

(2) Taasisi inaweza, kwa madhumuni ya matumizi ya kibiashara au matumizi ya ugunduzi au ubunifu wowote na kutumika kwake, kuafikiana na mtu kununua,

kuuza, kuchukua au kumpa haki miliki za ubunifu kwenye ugunduzi au ubunifu kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Sera ya Mali Bunifu ya Taasisi.

(3) Taasisi itasajili kila ugunduzi au ubunifu uliopatikana kutokana na matokeo ya utafiti uliofanywa chini ya Sheria hii.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Taasisi inaweza kumzawadia mtu aliyehusika na ugunduzi au ubunifu.

(5) Taasisi itaandaa na kuendeleza Sera ya Mali Bunifu inayohusiana na utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu.

Taarifa.

**22**.-(1) Mtu anayejihusisha na utafiti wa kilimo, mifugo au rasilimali za misitu, kwa gharama zake, atawasilisha kwa Taasisi taarifa zinazohusiana na utafiti wake na ataipatia Taasisi nakala za kumbukumbu na ugunduzi wowote kama itakavyoelekezwa na Taasisi.

(2) Taasisi itahakikisha usiri wa taarifa zote za utafiti zilizowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Mtu ambaye atakiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

Uchapishaji wa matokeo ya utafiti.

**23**.-(1) Mtafiti ambaye anakusudia kuchapisha au anasababisha kuchapishwa matokeo ya utafiti atawasilisha nakala ya rasimu kwa Mkurugenzi Mkuu kwa ajili ya kuidhinisha.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu ataipitia rasimu hiyo na atakaporidhika, ataidhinisha kwa ajili ya kuchapishwa na ataweka nakala ya rasimu hiyo kwa ajili ya kumbukumbu.

(3) Mtu ambaye atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

Matumizi ya wanyama katika majaribio.

**24**.-(1) Mtafiti ambaye anakusudia kutumia mnyama katika majaribio ya utafiti ataomba ruhusa kwa Mkurugenzi Mkuu.

(2) Mkurugenzi Mkuu, baada ya kuridhika na kukamilishwa kwa masharti kama yalivyoainishwa katika kanuni, atatoa ruhusa kwa mtafiti kufanya majaribio.

(3) Masharti na namna ya kumtumia mnyama katika utafiti na mambo mengine yoyote yanayohusiana na hayo yataainishwa katika kanuni.

(4) Mtu ambaye atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

Uhamishaji wa sampuli.

**25.**-(1) Mtu anayekusudia kuhamisha sampuli yoyote kutoka au kuingia Zanzibar ataomba kibali kwa Mkurugenzi Mkuu.

(2) Mkurugenzi Mkuu, baada ya kuridhika kukamilishwa kwa masharti kama yalivyoainishwa katika kanuni, atatoa kibali kwa muombaji.

(3) Mtu ambaye atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

## SEHEMU YA TANO
## KUANZISHWA KWA KAMATI YA MAADILI YA UTAFITI

Kuanzisha na muundo wa Kamati ya Maadili ya Utafiti.

**26.** -(1) Kutakuwa na Kamati ya Maadili ya Utafiti ya Taasisi ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti;

(b) wakuu wa Idara za Taasisi;

(c) mjumbe mmoja kutoka sekta ya kilimo;

(d) mjumbe mmoja kutoka sekta ya mifugo; na

(e) mjumbe mmoja kutoka sekta ya rasilimali za misitu.

(2) Wajumbe chini ya kifungu kidogo cha (1)(a), (c), (d) na (e) cha kifungu hiki watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kulingana na sifa zao na uzoefu.

(3) Katibu wa Bodi atakuwa Katibu wa Kamati.

(4) Masharti ya mwenendo wa Bodi yanayofaa yatatumika kwa Kamati ya Maadili ya Utafiti.

Kazi za Kamati ya Maadili ya Utafiti.

**27.** Kamati ya Maadili ya Utafiti:

(a) itapitia na kuidhinisha mapendekezo yote ya miradi ya utafiti itakayofanywa Zanzibar kwa kuzingatia maadili;

(b) itatayarisha miongozo na utaratibu wa kuomba idhini ya kimaadili kutoka katikaTaasisi;

(c) itapitia mapendekezo ya miradi ya utafiti utakaofanywa na Taasisi au mtafiti binafsi kwa kuzingatia misingi ya kitaalamu na kifedha na kuwasilisha kwa Mkurugenzi Mkuu;

(d) itapitia nyaraka zote za kisayansi za utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu utakaofanywa na Taasisi na kutoa idhini kabla ya kuchapishwa;

(e) itaandaa mikutano ya mwaka, semina na makongamano ya mapitio ya utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu kwa wadau; na

(f) itafuatilia na kutathmini maendeleo ya utafiti utakaofanywa na Taasisi na kuwasilisha matokeo yake kwa Bodi.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha na Rasilimali za Taasisi

**28**.-(1) Fedha na rasilimali za Taasisi zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha zozote halali zilizopokelewa na Taasisi kutokana na huduma zinazotolewa na Taasisi;

(c) misaada halali, zawadi, ufadhili, michango, mikopo, urithi au uwekezaji kama Taasisi itakavyopokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote; na

(d) fedha nyengine zozote ambazo zinaweza kupewa au kupatikana kihalali na Taasisi wakati wa utekelezaji wake au vyenginevyo.

(2) Taasisi itatekeleza kazi zake kwa mujibu wa misingi ya kifedha iliyopo na itahakikisha kwamba mapato yake yanajitosheleza kufikia matumizi yake ipasavyo.

(3) Taasisi inaweza kubakiza asilimia fulani ya fedha zilizokusanywa kama itakavyoamuliwa na Waziri anayehusika na Fedha.

(4) Miamala yote ya fedha za Taasisi itafanywa na itasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

Bajeti ya Taasisi

**29**.-(1) Mkurugenzi Mkuu, katika kila mwaka wa fedha, ataandaa na kuwasilisha kwa Bodi kwa ajili ya majadiliano na mapendekezo ya makadirio ya kina ya mapato na matumizi ya Taasisi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Baada ya majadiliano na mapendekezo ya Bodi, bajeti ya Taasisi itachukuliwa kuwa sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Makadirio ya mapato na matumizi ya Taasisi yataandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016 na miongozo mingine yoyote itakayotolewa na Serikali kila baada ya muda.

(4) Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba malipo yote yanayofanywa kwa fedha za Taasisi ni sahihi na yanaidhinishwa ipasavyo.

Hesabu na Ukaguzi.

30.-(1) Taasisi itaweka na kutunza kwa usahihi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.

(2) Hesabu zote za Taasisi zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 na sheria nyengine zozote za fedha zinazohusika.

Uwezo wa kuwekeza

31.-(1) Taasisi inaweza, kwa mujibu wa sheria, kuwekeza sehemu yoyote ya fedha zake.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, fedha za faida zitakazotokana na uwekezaji zitatumika kwa madhumuni ya:

(a) maendeleo ya miundombinu ya utafiti, gharama za uendeshaji wa utafiti na kufanya biashara ya bidhaa za matokeo ya utafiti; na

(b) mafunzo au kuwajengea uwezo watumishi, wakulima, wafugaji au wahifadhi wa misitu wanaojihusisha na utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu.

Ripoti ya mwaka ya Taasisi.

32. Baada ya kupokea ripoti iliyokaguliwa kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkurugenzi Mkuu, ndani ya miezi mitatu atatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka wa fedha inayojumuisha:

(a) nakala ya hesabu zilizokaguliwa za Taasisi na taarifa ya mkaguzi inayohusika na hesabu hizo;

(b) ripoti ya Taasisi katika mwaka wa fedha; na

(c) taarifa nyengine kama Waziri anaweza kuzitaka au kuelekeza.

Ufunguaji wa hesabu za benki.

33. Taasisi, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, itafungua hesabu ya benki na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu.

**34**. Mtu ambaye

(a) anadanganya au anatoa taarifa isiyo sahihi ambayo inazuia utekelezaji wa kazi za utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu;

(b) anaingilia au anasababisha kuingilia ufanyaji wa utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu;

(c) anamzuia au anamkwaza mtafiti katika kutekeleza majukumu yake;

(d) anahaulisha matokeo ya utafiti wake mahali pengine bila ya ruhusa ya Mkurugenzi Mkuu;

(e) anaharibu au anaathiri mali au kazi yoyote inayohusiana na utafiti; au

(f) anashindwa kuzingatia masharti ya vifungu vya 18,19, 20, 22 23, 24 na 25 vya Sheria hii,

ametenda kosa, na akitiwa hatiani:

(i) ikiwa ni mtu binafsi, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja na isiyozidi Shilingi Milioni Mbili, au kifungo kwa kipindi cha miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo, na ikiwa ni kosa linalojirejea, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili na isiyozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo cha miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili; na

(ii) ikiwa ni shirika au taasisi, litalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano, na ikiwa ni kosa linalojirejea, litalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi.

Adhabu ya ziada.

**35**. Mtu yeyote atakapotiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria hii, Mahakama, mbali na adhabu aliyopewa chini ya Sheria hii, itaamuru iwapo mali za utafiti au utafiti umeharibiwa, umeathiriwa au umeondolewa kwa dhamira ya kutenda kosa, mtu huyo atalipa fidia inayofanana na thamani ya uharibifu alioufanya.

Kumaliza kosa.

**36**.-(1) Mkururgenzi Mkuu anaweza kumaliza kosa lililofanywa na mtu chini ya Sheria hii au kanuni zake kwa kumtaka kulipa faini isiyopungua nusu ya faini iliyoainishwa kwa kosa hilo, iwapo mtu huyo:

(a) amekubali kwamba ametenda kosa;

b) atalipa malipo yote ya msingi chini ya Sheria hii.

(2) Taratibu zinazohusiana na kumaliza kosa zitaainishwa katika kanuni.

(3) Kumaliza kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hakutochukuliwa kama ni hatia kwa kosa linaloshukiwa kufanywa na isipokuwa kwamba malipo ya msingi yamelipwa yote, hakutokuwa na mashtaka kwa kosa linaloshughulikiwa ambalo litafunguliwa au kuendelezwa.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Rufaa.

**37.**-(1) Mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Mkurugenzi Mkuu kuhusu utekelezaji wa masharti ya Sheria hii anaweza, ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea uamuzi huo, kukata rufaa kwa Bodi.

(2) Bodi itaipitia rufaa hiyo na kutoa uamuzi ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ya kupokea rufaa hiyo.

(3) Mtu asiyeridhika na uamuzi chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, anaweza ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea uamuzi huo kukata rufaa kwa Waziri ambaye ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ya kupokea rufaa hiyo atatoa uamuzi.

Uwezo wa kurekebisha Jadweli

**38.** Waziri anaweza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, kurekebisha Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

Kanuni.

**39.**-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri uwezo wa jumla wa masharti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri atatunga kanuni kuhusiana na:

(a) utaratibu wa usajili wa watafiti na watoa huduma za utafiti;

(b) kueleza namna ya kulinda haki miliki ya ubunifu ya ugunduzi au ubunifu inayotokana na utafiti;

(c) malipo ya ada na tozo zinazolipwa chini ya Sheria hii;

(d) utaratibu wa uchapishaji wa matokeo ya utafiti;

(e) uwekaji wa viwango na kanuni za maadili ya utafiti;

(f) utaratibu wa kuomba idhini ya maadili ya utafiti;

(g) utaratibu wa kufanya majaribio ya wanyama;

(h) utaratibu wa kuwasilisha kwa Taasisi mapendekezo ya utafiti; na

(i) utaratibu na namna ya uhifadhi wa taarifa za utafiti wa kilimo, mifugo na rasilimali za misitu.

Kufuta na kubakiza.

**40**.-(1) Sheria zifuatazo zinafutwa:

(a) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar. Nam. 7 ya 2020; na

(b) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Nam. 8 ya mwaka 2020.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya sheria zilizofutwa litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

---

## MAENEO YA UTAFITI
**[Chini ya kifungu cha 5(2)(a)]**

---

1. Upandishaji kwa njia ya sindano na uhamishaji wa mimba
2. Bioteknolojia
3. Uhimilivu na upunguzaji wa athari za mabadiliko ya tabianchi
4. Mazao
5. Misitu
6. Benki za vinasaba
7. Vyanzo vya vinasaba
8. Uzalishaji wa vifaranga
9. Usimamizi wa pembejeo
10. Mifugo
11. Maarifa ya asili katika uzalishaji na usimamizi
12. Kilimo hai
13. Malisho na chakula cha wanyama
14. Wadudu na maradhi
15. Usindikaji, uhifadhi, matumizi na masoko ya bidhaa
16. Uzalishaji
17. Uzalishaji wa mbegu na miche
18. Masuala ya kijamii na kiuchumi katika kilimo na mifugo
19. Afya ya jamii inayohusiana na wanyama
20. Wanyama na mazingira pori
21. Udongo
22. Mambo mengine yoyote yanayohusiana na kilimo, mifugo na rasilimali za misitu.

## JADWELI LA PILI

---

## MWENENDO WA BODI
**[Chini ya kifungu cha 11]**

---

Makamu Mwenyekiti.

**1.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Muda wa wajumbe.

**2.** Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

**3.**-(1) Bodi itakutana kikawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana kwa ajili ya kikao cha dharura muda wowote kila itakapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

(2) Mwenyekiti ataendesha vikao vyote vya Bodi, na ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha vikao vya Bodi na ikiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliohudhuria watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

**4.** Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wa Bodi wataunda akidi katika kikao cha Bodi.

Uamuzi wa Bodi.

**5.** Uamuzi wa Bodi utafanywa kwa maafikiano, na endapo hakuna maafikiano, uamuzi utafanywa kwa kura, na endapo ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Taratibu za vikao.

**6.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake.

Mjumbe mualikwa.

**7.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya vikao vya Bodi kama mtaalamu, lakini mjumbe mualikwa huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kamati za Bodi.

**8.** Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati pale inapoona inafaa.

Kukasimu kazi za Bodi.

**9.**-(1) Bodi inaweza, itakapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati za Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa maelekezo kwa maandishi kama itakavyoona muhimu kuhakikisha utekelezaji bora wa kazi zake.

Posho la Wajumbe.

**10.** Wajumbe wa Bodi watastahili kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

Kubainisha maslahi.

**11.**-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi binafsi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo ambalo linalohusika au linalotakiwa kujadiliwa na Bodi, haraka iwezekanavyo, baada ya kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha maslahi hayo:

(a) hatohudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya maamuzi; au

(b) hatomshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya maamuzi.

Kusita kuwa Mjumbe.

**12.** Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu ya msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili;

(d) ikiwa atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza mjumbe huyo;

(e) ikiwa atasitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Taasisi; au

(f) kifo.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 11 Septemba, 2024.

..........................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***